

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Anwani ya Simu "ADMIN"
WILAYA,
Simu ya Mdomo: 2540484/2540054
Fax. No. 025-2540332.
Unapojibu tafadhali taja:



OFISI YA MKUU WA
S.L.P. 44,
KYELA.

Kumb. Na. AB.297/373/01/40

28/08/2022

KWA WANANCHI WOTE.

YAH: UANDIKISHAJI WA VIJANA WA KUJIUNGA NA JESHI LA
KUJENGA TAIFA KWA UTARATIBU WA KUJITOLEA (HIARI) MWAKA
2022/2023

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya inawatangazia nafasi za kujiunga na Jeshi la kujenga Taifa kwa yoyote mwenye sifa zifuatazo :-


1. Awe raia wa Tanzania
2. Umri,
 - a. Kwa vijana wenye elimu ya darasa la saba umri ni kuanzia miaka 16 hadi 18
 - b. Vijana wenye elimu kidato cha nne umri usiwe zaidi ya miaka 20
 - c. Vijana wenye elimu ya kidato cha sita umri usiwe zaidi ya miaka 22
 - d. Vijana wenye elimu ya stahhada umri usiwe zaidi ya miaka 25
 - e. Vijana wenye elimu ya shahada umri usiwe zaidi ya miaka 26
 - f. Vijana wenye elimu ya shahada ya uzamili umri usiwe zaidi ya miaka 30.
 - g. Vijana wenye elimu ya shahada ya uzamivu umri usiwe zaidi ya miaka 35

3. Awe na afya njema, akili timamu na asiwe na alama yoyote ya michoro mwilini (Tattoo)
4. Awe mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia mahakamani na hajawahi kufungwa
5. Kwa vijana waliomaliza elimu ya sekondari kidato cha nne na sita wawe waliomaliza kuanzia mwaka 2019, 2020, 2021 na 2022 wenye ufaulu ufuatao:-
 - a) Wawe wamefaulu na wawe na alama (points) zisizopungua 32.
 - b) Vijana kidato cha sita wawe na ufaulu wa daraja la kwanza hadi la nne
6. Awe na cheti cha elimu ya msingi
7. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (original birth certificate)
8. Awe na cheti halisi cha kumaliza shule (school leaving certificate)
9. Awe na cheti halisis cha matokeo (original academic certificate/transcript)
10. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, chuo cha mafunzo au KMKM wala kuajiriwa na idara nyingine serikalini.
11. Asiwe amepitia JKT operesheni za nyuma.
12. Asiwe amejihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana na hayo.
13. Kwa wale wenye vipaji vya michezo mbalimbali na sanaa zitakuwa sifa za ziada pamoja na sifa za elimu zilizotajwa hapo juu.

Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo

MKUU WA WILAYA
S.L.P. 44
KYELA

Mwisho wa kutuma maombi hayo ni tarehe 01/09/2022


Godfrey C. Kawacha
**KATIBU TAWALA WILAYA
KYELA**